kufungua shauri katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.

Hata hivyo ikiwa mgogoro a Ardhi haujasuluhiswa kwa muda wa siku 30 tangu kuwasilishwa katika Baraza, na mtu asiyeridhika anaruhusiwa kwenda kufungua shauri katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya bila ya kuwa na hati.

3.3 Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya

Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya lina mamlaka ya kusikiliza migogoro yote ya ardhi kwa mujibu wa sheria mbalimbali za ardhi; kusikiliza mashauri ya mali isiyohamishika yenye thamani isiyozidi shilingi millioni mia tatu . Vilevile, Baraza lina mamlaka ya kusikiliza migogoro mingine ya ardhi ambayo inakadiriwa kuwa na thamani isiyozidi shilingi millioni 200. Aidha, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya linasimamia utekelezaji wa maamuzi yake.

3.4 Mahakama Kuu

Mamlaka ya Mahakama Kuu ni kusikiliza migogoro ya ardhi kwa mali isiyohamishika inayozidi shillingi millioni mia tatu; kusikiliza mashauri mengine ya ardhi yanayokadiriwa kuzidi shillingi millioni mia mbili; na kusikiliza rufaa kutoka Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.

Muda wa kupeleka rufaa ni siku 60 toka tarehe ya uamuzi. Hata hivyo ikiwa kuna sababu za msingi za kuchelewa Mahakama inaweza kuongeza muda wa kukata rufaa. Ikiwa mtu hajaridhika na uamuzi wa Mahakama Kuu anaweza kukata rufaa Mahakama ya Rufani.

3.5 Mahakama ya Rufani

Mahakama ya Rufani ni chombo cha juu katika utatuzi wa migogoro ya ardhi.Mahakama ya Rufani inapokea rufaa zinazotoka Mahakama Kuu.

4.0 Hitimisho

Migogoro ya ardhi inaathiri kwa shughuli za kiuchumi kiwango kikubwa na inachangia kuongezeka kwa mifarakano katika jamii. Katika utatuzi wa migogoro ya aridh, jamii inatakiwa kufuata taratibu zilizowekwa na sheria ili kudumisha amani katika Taifa hili.

Kwa Maoni, wasiliana na Tume kupitia anuani ifuatayo :

Katibu Mtendaji,
Tume ya kurekebisha Sheria Tanzania ,

Jengo la Taaluma Na. 1,
Barabara ya Mkalama
S.L. P 1718
DODOMA
TANZANIA

Barua pepe: lrct@lrct.go.tz
Tovuti: www.rlct.go.tz

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

UTATUZI WAMIGOGORO YA ARDHI

1.0 Utangulizi

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Tume) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kufanya mapitio ya sheria zote za Jamhuri ya Muungano na pia ina jukumu la kufanya tathmini ya utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia. Tume vilevile inajukumu la kutoa elimu ya sheria kwa Umma.

2.0 Sheria za Ardhi

Ardhi ya Tanzania imegawanyika katika makundi 3 ambayo ni **Ardhi ya kijiji, Ardhi ya Hifadhi** na **Ardhi ya Jumla**. Ardhi ya kijiji ni ardhi inalindwa na kusimamiwa na Sheria ya Ardhi ya Vijiji. Ardhi ya Hifadhi, hii ni ardhi iliyotengwa kwa matumizi maalum yenye faida kwa jamii. Ardhi hii ni pamoja na hifadhi za misitu, wanyamapori, maji, hifadhi za barabara na maeneo tengefu kama vile migodi, jeshi nk. **Ardhi ya Jumla** ni Ardhi ambayo inabaki baada ya kutoa ardhi hizo 2, na katika ardhi hii kuna ardhi za miji,halmashauri na majiji.

Sheria zinazosimamia masuala ya ardhi ni Sheria ya Ardhi, Sheria ya Ardhi ya Vijiji na Sheria ya Mahakama ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi.

Vyombo vyenye mamlaka ya kutatua migogoro ya ardhi ni:-

- Baraza la Ardhi la Kijiji,
- Baraza la Kata,
- Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya;
- Mahakama Kuu na
- Mahakama ya Rufani ya Tanzania.

3.0 Baraza la Ardhi la Kijiji

Baraza la Ardhi la Kijiji ni chombo cha chini katika utatuzi wa migogoro ya ardhi katika ngazi ya kijiji. Baraza hili linaanzishwa chini ya Sheria ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi. Baraza lina wajumbe 7 kati ya wajumbe hao 3 lazima wawe wanawake. Wajumbe wake huteuliwa na Halmashauri ya Kijiji na kuthibitishwa na Mkutano Mkuu wa kijiji.

3.1 Majukumu ya Baraza la Ardhi la Kijiji

Katika kutatua migogoro ya ardhi Baraza la Ardhi la Kijiji lina mamlaka yafuatayo:-

- Kupokea malalamiko ya ardhi toka kwa mwanakijiji mwenye malalamiko yanayohusu ardhi
- Kuitisha mikutano na kusikiliza migogoro ya ardhi kutoka kwa wanakijiji
- Kusuluhuisha na kusaidia wanakijiji walio na migogoro ya ardhi ili kufikia suluhu.

Baraza la Ardhi ya Kijiji baada kusililiza na kusuluhuisha mgogoro wa ardhi hutoa uamuzi wake na endapo wahusika hawajaridhika na hatua hiyo mgogoro huo unaweza kupelekwa kwenye Baraza la Kata

3.2 Baraza la Kata

Baraza la Kata ni chombo kimojawapo kati ya vyombo vilivyopewa mamlaka ya utatuzi wa migogoro ya ardhi. Baraza la Kata lina wajumbe wasiopungua 4 na wasiozidi 8 ambao miongoni mwao 3 lazima wawe wanawake. Idadi hii ni pamoja na Mwenyekiti wa Baraza. Wajumbe wa Baraza la Kata huteuliwa Hata hivyo katika usuluhishi Baraza hili litajumuisha watu 3 na ambao mmoja wapo lazima awe mwanamke

a) Sifa za mjumbe wa Baraza

Mtu yeyote atakuwa na sifa za kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Kata ikiwa mtu huyo ni

- Ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- Ana umri wa miaka 18 na kuendelea;
- Ni mkazi wa kata husika.

Mtu yeyote hastahili kuwa mjumbe katika Baraza la Kata ikiwa mtu huyo ni:-

- mjumbe wa Baraza la Ardhi la Kijiji, Halmashauri ya Kijiji au Kamati ya Maendeleo ya Kata;
- Mtumishi wa Umma;
- mwanasheria au mtu yeyote aliyeajiriwa Mahakamani;
- mbunge;
- ana matatizo ya akili;
- amewahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai linalohusiana na ukosefu au ukiukwaji wa maadili.

b) Majukumu ya Baraza la Kata

Katika kutatua migogoro ya ardhi, Baraza la Kata lina mamlaka ya kusuluhisha wahusika wenye migogoro ya ardhi ili waweze kufikia makubaliano.

Usuluhishi unaposhindikana, Baraza linatakiwa kutoa hati kuwa mgogoro umeshindikana kusuluhishwa ili mhusika aweze kwenda